# NATION MEDIA GROUP PLC

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

Taarifa inatolewa hapa kuwa Mkutano Mkuu wa Sitini na Tatu wa Kila Mwaka wa Wenyehisa wa Shirika la Nation Media Group PLC utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Ijumaa, tarehe 26 Juni 2026 kuanzia saa tisa kamili alasiri EAT ili kufanya shughuli zilizo hapa chini.

*Maamuzi yote yatafanywa kwa kupigiwa kura.*

**SHUGHULI ZA KAWAIDA**

**1.** Kupokea taarifa za kifedha za mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2025, pamoja na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi wa Hesabu za Fedha.

**2.** Kufahamu kwamba Wakurugenzi hawapendekezi mgao wa faida katika mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2025.

**3.** Kupokea, kuzingatia na ikiwa inafaa, kuidhinisha Ripoti ya Malipo ya Wakurugenzi na malipo waliolipwa Wakurugenzi kwa kipindi kilichokamilika tarehe 31 Desemba 2025 na kuipa Bodi mamlaka ya kuamua malipo ya Wakurugenzi Wasio Watendaji.

**4.** Kuthibitisha kwamba Wakaguzi wa Hesabu za Fedha, Kampuni ya PricewaterhouseCoopers LLP, kwa kuwa wameonyesha nia, wataendelea kufanya kazi kama Wakaguzi wa Hesabu za Fedha wa Kampuni hii kwa mujibu wa kipengee cha 721(2) cha Sheria ya Kampuni za Kenya, Sura ya 486, Sheria za Kenya na kuwapa Wakurugenzi mamlaka ya kuamua malipo ya Wakaguzi hao wa Hesabu za Fedha ya mwaka ujao.

**5.** Kuchagua tena Wakurugenzi:

a) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Sultan Allana anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;

b) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Fayyaz Nurmohamed anastaafu kwa zamu na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena;

c) Kwa mujibu wa Kifungu cha 110 cha Katiba ya Kampuni, Bw. Dennis Aluanga anastaafu kwa zamu na hatawania kuchaguliwa tena;

d) Bw. Al-Noor Ramji, kwa kuwa amefikisha umri wa miaka 70, anastaafu kwa zamu, na kwa kuwa ametimiza masharti, anajitolea kuchaguliwa tena.

**6.** Kuteua wanachama wa Kamati ya Ukaguzi wa Kampuni na Kamati ya Hatari na Uzingatiaji:
Kwa mujibu wa kipengee cha 769 (1) cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 486, Sheria za Kenya, Wakurugenzi wafuatao, kwa kuwa ni wanachama wa Kamati ya Ukaguzi wa Kampuni na Kamati ya Hatari na Uzingatiaji, wanachaguliwa tena ili kuendelea kuhudumu katika Kamati hizo:
a) Bw. David C Nchimbi
b) Bw. Al-Noor Ramji
c) Bw. Louis Otieno

**7.** Shughuli nyingine yoyote ambayo Taarifa halali itakuwa imetolewa.

**Kwa Amri ya Bodi,**

Angela Namwakira
Katibu wa Kampuni

4 Juni 2026

**MAELEZO**

1. Kwa mujibu wa kipengee cha 3 cha Sheria za Kampuni, Sura ya 486, Sheria za Kenya Zilizorekebishwa na Sheria ya Kanuni za Biashara (Marekebisho) (Na. 2), 2021, Mkutano Mkuu wa Sitini na Tatu wa Kila Mwaka wa Shirika la Nation Media Group PLC (''Kampuni'') utafanyika mtandaoni siku ya Ijumaa, tarehe 26 Juni 2026 saa tisa kamili alasiri.

2. Wenyehisa ambao wangependa kushiriki katika mkutano huo wanapaswa kujiandikisha mtandaoni kupitia https://digital.candr.africa/ au kwa kubofya nambari hizi za USSD kwenye simu ya mkononi; *483*420# au kupitia kwa kiungio (linki) ya Jukwaa la Mkutano Mkuu wa Mwaka ambayo watatumiwa kupitia kwa ujumbe mfupi wa SMS na/au Baruapepe na kufuata maelekezo kuhusu harakati ya kujisajili. Ili kukamilisha harakati hiyo ya kujisajili, wenyehisa watahitajika kukumbuka Nambari za Kitambulisho/Pasipoti ambazo zilitumika kununua hisa zao na namba zao za akaunti ya hisa au Namba za Akaunti ya CDSC.

3. Harakati ya kujisajili kwa Mkutano Mkuu wa kila Mwaka itafunguliwa tarehe 15 Juni 2026 saa tatu kamili asubuhi na kufungwa tarehe 25 Juni 2026 saa sita adhuhuri.

4. Kwa usaidizi, wenyehisa wanaombwa kupiga nambari ifuatayo ya usaidizi: +254 20 8690360 kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na nusu jioni kipindi ambacho harakati ya kujisajili itakuwa imefunguliwa. Mwenyehisa yeyote aliye nje ya Kenya anaombwa kupiga nambari hiyo ya usaidizi ili kupata usaidizi wa kujisajili au kutuma baruapepe kwa digital@candr.africa.

5. Kwa mujibu wa Kipengee cha 283 (2)(c) cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 486, nakala zifuatazo zinaweza kutazamwa kwenye tovuti ya Kampuni hii: https://www.nationmedia.com

   a. nakala ya Notisi hii na Fomu ya Uwakilishi;
   b. Taarifa za Kifedha za Kampuni hii Zilizokaguliwa za mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2025;

6. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali yoyote kuhusu Mkutano Mkuu wa Mwaka wanaweza kufanya hivyo kwa:
   (i) Kutumia kiungio kilichotumwa kwa njia ya sms/baruapepe baada ya kuthibitisha usajili; au
   (ii) Kutembelea Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kupitia: https://digital.candr.africa/ au kupitia kwa kiungio cha jukwaa la Mkutano Mkuu wa Mwaka; Nenda kwa kichupo cha Attend Event; Kisha Chagua “Nation Media Group Plc AGM”; Kisha “Q&A” halafu wasilisha maswali kwa kisanduku kilichotolewa; au
   (iii) Kutembelea Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kwa kubonyeza nambari ya USSD kwenye simu ya mkononi; *483*420#; Fuata maelekezo ya menyu ili kuchagua “Q&A” na wawasilishe maswali yako (ujumbe mmoja wa sms usizidi maneno 160); au
   (iv) Kutuma maswali yaliyoandikwa kwa baruapepe: digital@candr.africa au
   (v) Kama inawezekana, kuwasilisha moja kwa moja maswali yaliyoandikwa na anwani ya mahali au ya baruapepe ya kurejesha majibu, katika afisi za Msajili wa Kampuni hii, Custody and Registrars Service Ltd, IKM Place, Tower B, Orofa ya 1, 5TH Ngong Avenue. Wenyehisa wanaotuma maswali yao kwa baruapepe au kuwasilisha kwa kampuni ya C&R Group sharti watoe maelezo yao kamili (majina kamili, Namba ya Akaunti ya Hisa/ Namba ya Akaunti ya CDSC) wanapowasilisha maswali na ufafanuzi wao. Pia waambatanishe nakala ya Kitambulisho/ Pasipoti.

   **Maswali kupitia kwa tovuti ya Mkutano Mkuu wa Mwaka**

   Wenyehisa wataweza kuuliza maswali kwenye jukwaa la Mkutano Mkuu wa Mwaka la mtandaoni kabla na wakati wa Mkutano huo, wakitumia tovuti au nambari ya USSD.

   **Maswali ya Moja kwa Moja Mtandaoni Mkutano Mkuu wa Mwaka Ukiendelea**

   Wenyehisa watapata nafasi ya kufuatilia Mkutano Mkuu wa Mwaka mtandaoni na kuuliza maswali yao wakati wa mkutano huo. Wenyehisa ambao wangependa kuuliza maswali mtandaoni wakati Mkutano huo ukipeperusha moja kwa moja wanaweza kujiunga (kwa kuchagua kichupo cha “Join AGM Meeting Room” chini ya skrini ya picha za moja kwa moja). Wakishajiunga, wenyehisa wanaweza kuendelea kutazama matangazo ya Mkutano huo na i) kuchagua “raise hand” kwenye skrini zao ili kuomba nafasi ya kuuliza maswali yao kwa Bodi au ii) kuandika maswali kwenye gumzo la moja kwa moja mtandaoni ili kusomwa na Bodi wakati wa Mkutano huo.

7. Wenyehisa ambao wangependa kupiga kura wanaweza kufanya hivyo kwa:
   (i) Kutembelea Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kupitia: https://digital.candr.africa/ au kupitia kwa kiungio cha jukwaa hilo; Nenda kwa Attend Event; Chagua “Nationa Media Group Plc AGM”; Kisha chagua kichupo cha “Voting” na upige kura yako; au
   (ii) Kutembelea Mkutano Mkuu wa Mwaka Mtandaoni kwa kubonyeza nambari za USSD zifuatazo; *483*420#; Fuata maelekezo kwenye menyu kisha Chagua “Voting” halafu fuata maelekezo kadhaa kuhusu harakati ya kupiga kura.

8. Kwa mujibu wa Kipengee cha 298(2) cha Sheria za Kampuni, Sura ya 486, walio na haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika Mkutano Mkuu wa kila Mwaka wana haki ya kuteua mwakalishi wa kupiga kura kwa niaba yao. Si lazima mwakilishi huyo awe mwanachama wa Kampuni hii lakini mwenyehisa asipoteua mwakilishi wake, Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Mwaka atamwakilisha. Fomu ya uwakilishi imeambatinishwa kwenye Notisi hii na pia inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni hii: https://www.nationmedia.com.. Nakala za karatasi za fomu ya uwakilishi pia zinapatika katika anwani ifuatayo:

   **Afisi za Custody and Registrars Services,**
   **IKM Place, Tower B, Orofa ya 1,**
   **5th Ngong Avenue.**

   Ili kuwa halali, fomu ya uwakilishi inapaswa kujazwa na mwenyehisa, au wakili wake aliyeidhinishwa kwa maandishi. Ikiwa mwanachama ni shirika, idara inayoteua mwakilishi huyo sharti itie muhuri wa shirika hilo (ikiwa kuna wowote) au saini ya afisa au wakili aliyeidhinishwa wa shirika hilo.

   Fomu ya uwakilishi iliyojazwa inafaa kutumwa kupitia kwa baruapepe proxy@candr.africa kwa mtindo wa pdf au kuwasilishwa kwa Kampuni ya Custody and Registrars Services, IKM Place, Tower B, Orofa ya 1, 5th Ngong Avenue Nairobi au kutumwa kwa anwani ya posta: Custody and Registrars Services, S.L.P. 8484-00100 Nairobi, ili kufikia Msajili au Katibu wa Kampuni hiyo kabla ya saa tisa alasiri, tarehe 24 Juni, 2026.

   Fomu hizo zilizojazwa sharti ziambatane na nakala ya Kitambulisho/Pasipoti ya mwenyehisa na Kitambulisho/Pasipoti, baruapepe au namba ya simu ya mwakilishi ili kusaidia katika usajili. Mwenyehisa husika atafahamishwa kuhusu kukatiliwa kwa usajili wowote wa mwakilishi wake kabla ya tarehe 25 Juni 2026 saa tisa kamili alasiri ili kutoa muda wa kushughulikia utata wowote uliopo.

9. Mkutano Mkuu wa Mwaka utaonyeshwa moja kwa moja mtandaoni kwa wenyehisa wote ambao watakuwa wamefanikiwa kujisajili.

10. Wenyehisa na wawakilishi waliosajiliwa kikamalifu watapokea ujumbe mfupi wa SMS/ na/au baruapepe masaa mawili kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kuanza, ili kuwakumbusha wenyehisa na wawakilishi waliojisajili kikamilifu kuwa Mkutano huo utaanza baada ya masaa mawili na kutoa kiungio cha kufuatilia moja kwa moja mtandaoni.

11. Wenyehisa na wawakilishi waliosajiliwa kikamilifu wanaweza kupiga kura (Wakiombwa kufanya hivyo na Mwenyekiti) kupitia nambari ya USSD *483*420# au kwa Jukwaa la Kufuatilia Mkutano Mkuu wa Mwaka.

12. Kura itapigwa kuhusu mapendekezo/maamuzi yote yaliyotolewa kwenye notisi.

13. Matokeo ya Mkutano huo yatachapishwa ndani ya saa 24 baada ya kukamilika kwake kwenye tovuti ya Kampuni hii: (www.nationmedia.com).

Kwa migao yoyote ya faida ambayo haijachukuliwa, njia inayotumika kulipa migao ya faida ya chini ya KShs 250,000 ni kupitia M-PESA. Wenyehisa ambao wangependa kupokea mgao wao kupitia M-PESA na hawajajisajili kwa huduma hiyo ya malipo wanaweza kubofya *483*038# ili kujisajili kwa migao ya siku zijazo au kuwasiliana na Msajili wa Hisa, Kampuni ya Custody & Registrars Services Limited.

Wenyehisa wote wa sasa na wa zamani wa Kampuni hii wanafahamishwa kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mali za Fedha ambazo Hazijachukuliwa Na. 40 ya 2011, Sehemu ya II na III, migao ya faida na hisa ambayo haijachukuliwa na wenyewe kwa muda wa miaka mitatu (3) au zaidi itahitajika kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mali za Fedha ambazo Hazijachukuliwa (“Mamlaka hiyo”) kama mali zilizotelekezwa, tarehe itakayoteuliwa.

Kwa hivyo, wenyehisa wa sasa na wa zamani ambao hawajachukua migao yao ya faida wanaombwa kuwasiliana kwa haraka na Msajili wa Hisa, Kampuni ya Custody & Registrars Services Limited katika anwani iliyo hapa chini ili kudai migao yoyote ya faida na kuepuka hatari zitakazotokana na migao yao kupelekewa kwa Mamlaka hiyo.

**Custody & Registrars Services Ltd (C&R Group)**
**IKM Place, Tower B, Orofa ya 1**
**5th Ngong Avenue, Nairobi**
**Simu + 254 20 760 8216**